**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

CHUO CHA MAFUNZO YA UFUGAJI NYUKI - TABORA

**S.L.P. 62, TABORA, TANZANIA**
**Simu: +255 (0) 26 2605058**
**Nukushi: +255 (0) 26 2605338**
**BaruaPepe:*info@bti.ac.tz***
**Tovuti*: www.bti.ac.tz***

Kumb. Na. B/TRA/I/VOL. III/08 02/03/2015

## NAFASI ZA KUJIUNGA NA KOZI YA UFUGAJI NYUKI KWA MWAKA WA MASOMO 2015/2016

Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora kinatangaza nafasi za masomo kwa mwaka wa masomo 2015/2016 katika ngazi ya Stashahada na Astashahada.

**Kozi zinazotangazwa**

i. Astashahada ya Ufugaji Nyuki: Mafunzo ya miaka miwili (2) (NTA - Level 5)

ii. Stashahada ya Ufugaji Nyuki: Mafunzo ya miaka miwili (2) (NTA – Level 6)

### A. Sifa za Mwombaji:

**Kozi ya Astashahada ya Ufugaji Nyuki (Cheti)**

i. Mwombaji awe amemaliza kidato cha nne na awe amefaulu na kupata angalau alama D zisizopungua nne katika masomo ya Hisabati, Biolojia, Fizikia, Kemia, Jiografia, Sayansi Kilimo na Kingereza.

**Kozi ya Stashahada ya Ufugaji Nyuki (Diploma)**

i. Awe amemaliza kidato cha sita na awe amefaulu na kupata angalau alama E isiyopungua moja na subsidiary moja katika masomo ya Hisabati, Biolojia, Kemia, Jiografia, Fizikia na Sayansi Kilimo.

**AU**

Mwombaji awe amemaliza na kufaulu mafunzo ya Astashahada (cheti) katika fani ya Ufugaji Nyuki, Misitu, Wanyamapori, Kilimo au Mafunzo ya Astashahada yanayolandana na taaluma ya ufugaji nyuki kutoka kwenye chuo kinachotambulika na kupata angalau daraja la pili.

### B. Ada

Waombaji watakaochaguliwa watatakiwa kulipa ada kama ifuatavyo:

- **Kwa Wanafunzi wa Bweni**

i. Mwaka wa Kwanza: **Astashahada na Stashahada** Sh 1,700,000/= (kati ya hizo ada ya mafunzo ni sh 530,000/= na chakula na malazi ni sh 1,170,000/=)

ii. Mwaka wa Pili:

- **Astashahada** Sh 2,005,000/= (kati ya hizo ada ya mafunzo ni Sh 835,000/= na chakula na malazi ni Sh 1,170,000/=);

- **Stashahada** Sh 2,085,000/= (kati ya hizo ada ya mafunzo ni Sh 915,000/= na chakula na malazi ni Sh 1,170,000/=)

❖ **Kwa Wanafunzi wa Kutwa**

i. Mwaka wa Kwanza: **Astashahada na Stashahada** Sh 1,030,000/= (kati ya hizo ada ya mafunzo ni Sh 530,000/= na chakula ni Sh 500,000/=)

ii. Mwaka wa Pili:
   - **Astashahada** Sh 1,335,000/= (kati ya hizo ada ya mafunzo ni Sh 835,000/= na chakula ni Sh 500,000/=);
   - **Stashahada** Sh 1,415,000/= (kati ya hizo ada ya mafunzo ni Sh 915,000/= na chakula ni Sh 500,000/=) **N.B.** Mwanafunzi wa kutwa anachangia huduma ya chai na chakula cha mchana.

Ada yaweza kulipwa kwa awamu tatu – nusu mwanzo wa muhula wa kwanza, robo mwanzo wa muhula wa pili na robo ya mwisho katikati ya muhula wa pili.

**C. Jinsi ya Kutuma maombi**

i. Mwombaji atatakiwa kujaza fomu ya maombi ambayo italipiwa **Sh 20,000/=**

ii. Maombi yote yaambatanishwe na vivuli vya vyeti halisi pamoja na nakala halisi ya hati ya malipo ya benki (Pay –in Slip) kwa ajili ya fomu. Iwapo mwombaji ana ufadhili wa tasisi yoyote, anapaswa kuambatanisha barua ya uthibitisho kutoka kwa mfadhili wake;

iii. Fomu za maombi zinapatikana Chuoni na kwenye Tovuti ya Chuo; www.bti.ac.tz

**D. Mwisho wa kutuma maombi**

Mwisho wa kutuma maombi ni Tarehe **30 Aprili 2015**. Aidha, maombi yatakayotumwa baada ya tarehe iliyotajwa hayatafikiriwa.

**Maombi yote yatumwe kwa:**

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki,
S.L.P 62
**TABORA.**
Barua pepe: info@bti.ac.tz

**E. Taarifa kwa watakaochaguliwa.**

Majina ya watakaochaguliwa yatatangazwa kwenye magazeti na kwenye tovuti ya Chuo **(www.bti.ac.tz)**

Tangazo hili limetolewa na:

**Mkuu wa Chuo, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki**
**Kny: Katibu Mkuu**

**Wizara ya Maliasili na Utalii**